TUNDURU AGRICULTURAL MARKETING CO-OPERATIVE UNION
(TAMCU LTD REG. NO. 5490)

TELEPHONE NO. 025-2680850
Email: tamcutunduru@gmail.co

P.O.BOX 299
Tunduru –
Ruvuma

TAARIFA YA UFUNGUZI KWA MINADA YA MBAAZI MSIMU WA MWAKA 2023/2024

1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015 pamoja na Masharti ya TAMCU Ltd baadhi ya madhumuni ya Chama Kikuu ni pamoja na:

a) Kununua, kuuza na kusambaza pembejeo za kilimo kwa wanachama wake kwa bei nafuu;
b) Kukusanya na kuuza mazao kwa lengo la kuyauza kwa faida ya wanachama wake;
c) Kuanzisha na kuendeleza mitandao mizuri na imara ya kilimo bora cha mazao ya kilimo;
d) Kutoa elimu ya Ushirika kwa wanachama wake na kuwaendeleza Watendaji wa Chama ili kuleta ufanisi mzuri na kuimarisha uchumi wa chama; na
e) Kufanya mambo mengine yaliyo halali na ambayo ni ya lazima katika kuendeleza kazi zilizotajwa hapo juu katika kufanikisha utekelezaji wa dhumuni la Chama kama yatakavyopitishwa na Mkutano Mkuu.

2.0 MALENGO WA UKUSANYAJI WA MBAAZI MSIMU WA 2022/2023

Msimu wa mwaka 2022/2023 Chama Kikuu kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika vya Msingi wilayani Tunduru vilijiwekea malengo ya kukusanya mbaazi kilo **5,451,000**. Aidha, kutokana na sababu ambazo zipo nje ya uwezo wetu tulikusanya kilo **3,035,692** ambazo ni pungufu kwa kilo **2,415,308** sawa na anguko la asilimia **44.31%** ya lengo la ukusanyaji.

3.0 MAUZO YA MBAAZI KWA MSIMU WA 2022/2023

Zao la mbaazi katika Msimu wa mwaka 2022/2023 liliendelea kuuzwa kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Jumla ya minada sita (**06**) ya mauzo ya Mbaazi ilifanyika ambapo Kilo **3,035,692** ziliuzwa zenye thamani ya Tshs **2,633,233,690.00/-** *(angalia jedwali la mauzo ya Mbaazi hapo chini)*

NA.	TAREHE	NAMBA YA MNADA	KIASI KILICHOUZWA	BEI (JUU &CHINI)	BEI	THAMANI
1	30.08.2022	1	1,592,303	950 855	886.51	1,411,592,533
2	08.09.2022	2	551,429	815 780	798.00	440,040,342
3	15.09.2022	3	432,805	800 800	800.00	346,244,000
4	22.09.2022	4	212,929	785 875	875.00	186,312,875
5	06.10.2022	5	210,658	1,100 1,100	1,010.00	212,768,580
6	19.10.2022	6	35,568	1,020 1,020	1,020.00	36,279,360
JUMLA			**3,035,692**			**2,633,237,690**

Aidha, ukusanyaji wa zao la Mbaazi umepungua kidogo kutoka Kilo **4,111,845** msimu wa 2021/2022 hadi kilo **3,035,692** msimu wa 2022/2023 ambapo ni sawa na anguko la asilimia **26.17%** la Ukusanyaji katika mauzo.

Bei ya zao la Mbaazi msimu wa 2022/2023 ilishuka ambapo bei wastani ilikuwa ni **898.25/-** ukilinganisha na **1,264/-** ya msimu wa 2021/2022.

4.0 MAKISIO YA UKUSANYAJI WA MBAAZI MSIMU WA 2023/2024

Chama Kikuu kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa msimu wa mwaka 2023/2024 kimejiwekea malengo ya kukusanya Mbaazi kilo **5,350,788**.

5.0 HALI YA UPATIKANAJI WA VIFUNGASHIO (VIROBA) KWA MSIMU WA MSIMU 2023/2024

Kwa msimu wa mazao wa 2023/2024 Chama kikuu kimeagiza viroba **130,000** Kwa ajili ya Mbaazi na tayari viroba hivyo vimeshafika TAMCU Ltd. Aidha, kwenye Ufuta tumebakiwa na bakaa ya viroba **15,000** hivyo, tuna vifungashio vya kutosha ambavyo vinaweza kuhifadhi mbaazi zaidi ya Kilo **7,250,000**.

6.0 MAFANIKIO

Katika msimu wa mauzo ya Mbaazi Chama Kikuu kimepata mafanikio kadhaa kama yalivyoanishwa hapa chini: -

i. Kufanikisha Usimamizi wa mauzo ya Mbaazi kupitia mfumo wa Stakabadhi ghalani, ambapo wadau mbalimbali zikiwepo taasisi za Serikali zimeweza kupata ushuru stahiki kutokana na uwepo wa takwimu sahihi;
ii. Tumefanikisha kufanya malipo ya Zaidi ya Tsh. 2,633,233,690.00 kwa wakulima na wadau wengine;
iii. Tumefanikiwa kuondoa changamoto ya vifungashio kwa zao la mbaazi kwa kuhakikisha vinapatikana wakati wote wa biashara ya mbaazi; na

iv. Kufanikisha upatikanaji wa wasafirishaji ambao waliwezesha mazao ya wakulima kutoka maeneo mbalimbali ya Tunduru kufika katika Ghala kuu la mnada kwa wakati.

7.0 CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio tuliyopata katika msimu wa Mbaazi, pia zipo changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa msimu wa mbaazi; -

i. Changamoto ya kuchelewa kutoka maamuzi juu ya mfumo ambao ungetumika kuuza mbaazi msimu wa 2022/2023 na kupelekea utoroshwaji wa mbaazi, hivyo kupoteza mapato na kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mbaazi kwa msimu wa 2022/2023 kwa asilimia 44.31%;
ii. Utoroshwaji wa Mbaazi ambao kwa asilimia kubwa ni kutokana uwepo mfumo wa mauzo huria kwa mikoa Jirani;
iii. Kushuka kwa bei ya Mbaazi katika minada, msimu wa 2022/2023 bei ya Mbaazi katika minada zilikuwa zipo chini ukitofautisha na msimu uliopita wa mwaka 2021/2022. Mathalani msimu uliotangulia wa 2021/2022 bei wastani ilikuwa 1,264 ukilinganisha na bei ya Tsh. 898.25; na
iv. Akaunti za wakulima kutokuwa hai, changamoto ambayo imejitokeza pia kwa wakulima wengi akaunti zao kutokuwa hai. Hivyo, imepelekea malipo kwa wakulima husika kuchelewa.

8.0 RATIBA YA MINADA YA MBAAZI MSIMU WA 2023/2024

TAREHE	NAMBA YA MINADA	ENEO LA MNADA-KIJIJI	AMCOS HUSIKA
12/08/2023	1	Maji maji	Maji Maji
17/08/2023	2	Mbesa	Chichilimbe
24/08/2023	3	Msinji	Mndichana
31/08/2023	4	Angalia	Mshikamano
07/09/2023	5	Amani	Chamana
14/09/2023	6	Tuwemacho	Mlingoti Magharibi
21/09/2023	7	Ligunga	Ligunga
28/09/2023	8	Nakapanya	Namitili

9.0 KIASI KILICHOINGIA MNADANI

Kiasi kilichopelekwa Sokoni kwa mnada wa kwanza ni kilo **839,941** ya Mbaazi.

10.0 HITIMISHO

Mwisho, TAMCU inapenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa **Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Wakili. Julius Mtatiro** kwa kutusimamia na kutupatia ushauri wa mara mara ili kuendeleza shughuli za ushirika na tunakuomba uendelee kutusimamia na kutuongoza katika msimu huu wa 2023/2024.

Aidha, TAMCU inapenda kuwashurukuru Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Leseni ya Stakabadhi za Ghala, Mabenki, Wasafirishaji, Wanunuzi Pamoja na wadau wengine wote kwa kuendelea kushirikiana na sisi na tunawaomba muendelee kutoa ushirikiano kwa lengo la kusogeza mbele gurudumu la maendeleo.

NAOMBA KUWASILISHA

USHIRIKA PAMOJA TUJENGE UCHUMI

IMEANDALIWA NA
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA TUNDURU
12, AGOSTI 2023